

Transcript: Mchagua Jembe

- Baba: Nyamayao!
- Nyamayao: Bee, baba.
- Baba: Mwenzio yuko wapi?
- Nyamayao: Yupo, ndani.
- Baba: Muite haraka iwezekanavyo!
- Nyamayao: Rukia, unaitwa na baba.
- Rukia: Bee, baba.
- Baba: Wee, hata uso kunawa hujanawa.
- Rukia: Ndiyo, nataka kunawa baba.
- Baba: Sasa, wanangu kuna jambo moja nataka niwaambie, nataka muende shambani.
- Nyamayao: Kufanya nini baba?
- Baba: Mnajua mvua za masika zinaanza kunyeshu kwahiyo, nataka mwende shambani ili tuepukane na njaa sawa?
- Rukia na Nyamayao: Sawa baba, tutaenda.
- Baba: Nendeni mkabadilishe nguo haraka haraka ili muende shambani.
- Nyamayao na Rukia: Sawa, baba.
- Baba: Haya, nendeni.
- Nyamayao: Rukia, rudisha kikombe ndani ili twende shambani.
- Rukia: Ngoja, nikiweke hapa ili twende.
- Nyamayao: Acha jembe langu.
- Rukia: Hilo ni jembe langu, liache.

- Baba: Nendeni shambani, acheni kugombania jembe sawa.
- Rukia: Na leo, silimi na wewe.
- Nyamayao: Sawa, naenda mwenyewe hata usipolima na mimi.
Utakapolima wewe na mimi nalima hapo hapo.
Hili jembe sijui lina nini sijui ni butu?
- Rukia: Na wewe umeanza! jembe lina nini ?
Unavisingizio sana, nyumbani
umechagua hilo jembe mwenyewe
nikakuachia.
- Nyamayao: Kwanza, kichwa kinauma na nimechoka.
- Rukia: Yaani, wewe ndugu yangu ni mvivu hutaki kazi
yevote kwahiyio unataka nini?
- Nyamayao: Nataka hilo jembe lako kali.
- Rukia: Wewe, si ulichukua hilo jembe kali
nikakuachia?
- Nyamayao: Hilo jembe ni zito sana chukua hilo wewe.
- Rukia: Yaani wewe ni mvivu, hamna jembe zito wala
jepesi.
- Nyamayao: Hili nalo limewekwa kijiti sasa mimi
nitalimaje?
- Rukia: Hili shamba tutamaliza saa ngapi?
- Nyamayao: Mimi nimechoka bwana.
- Rukia: Baba akija mimi nitamueleza kila kitu,
umechoka nini unapenda kula tuu.
- Baba: Vipi, hapa wewe umekaa au unalima?
- Rukia: Baba, huyu ni mvivu sana.

Amechukua jembe langu akanipa la kwake,
alikua amekaa tuu sasa hivi ndiyo ameinuka.

Nyamayao: Baba,hili jembe ni zito sana.

Baba: Wewe, ni mvivu mtoto wangu.

Nyamayao: Hamna baba, hili jembe ni zito halafu baba
kichwa kinauma.

Rukia: Mtoto wako ni mvivu sana.

Nyamayao: Hamna baba, mikono yenye we imeota sugu
halafu inauma, heri ningebaki nyumbani
nioshe vyombo. Halafu baba, ungenunua
majembe mapya haya yamechoka lile jipya
halilimi vizuri.

Baba: Asubuhi, wewe si ndiye uliyetaka kubadilisha
jembe?

Nyamayao: Hilo jipya halilimi vizuri.

Baba: La zamani je?

Sasa, sikieni nyie nendeni nyumbani mimi
nitamalizia hapa.

Rukia: Mimi baba sifuatani naye.

Baba: Kwanini usifuatane naye?

Rukia: Yeye aende peke yake, na mimi nitaenda peke
yangu.

Nyamayao: Baba, mimi natangulia nyumbani.

Baba: Haya, tangulieni nyumbani.